

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA SABA

02 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA SABA – TAREHE 02 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA KILIMO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

217. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, kuna Wafanyakazi wangapi wanaofanya kazi za ndani nchini.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

218. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa Bwalo katika Shule ya Sekondari Nanyamba na kuwa ya Kidato cha Tano na Sita.

219. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Bwalo la Chakula, Majengo ya Utawala na Mabweni ya Wanafunzi katika Shule za Sekondari Misima na Handeni.

220. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Shule Maalum ya Sekondari ya Wasichana Dutumi Kata ya Bwakira Morogoro Vijijini.

221. MHESHIMIWA SIMON SONGE LUSENGEKILE (BUSEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Daraja linalounganisha Kijiji cha Lutubiga na Mwasamba - Busega.

WIZARA YA NISHATI:

222. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme katika Kijiji cha Lungunga Kata ya Ruakule - Kibiti.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

223. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ya Taaluma ya Ustawi wa Jamii ili kusimamia na kulinda Taaluma hii na kuwepo watoa huduma wenye leseni.

WIZARA YA KILIMO:

224. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanzisha Mfuko wa Kuimarisha Bei za Mazao ili kusaidia Wakulima wa Pamba na Mazao mengine bei zinaposhuka.

WIZARA YA UCHUKUZI:

225. MHESHIMIWA SANTIEL ERIC KIRUMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya ajira kwenye Miradi ya kimkakati ya SGR na ECOP kwa Mkoa wa Shinyanga.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

226. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaweka Kituo Kidogo cha Askari Wanyamapor Kata ya Mwangeza ili kudhibiti Tembo wanaofanya uharibifu kila mara.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA KILIMO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA
02 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**